

# Mlinda Mtoto Wako Dhidi ya COVID-19

## NAKALA

[muziki wa kulisimua]

[Simulizi]

Chanjo ya COVID-19 sasa inapatikana kwa watoto wenye umri wa miezi 6 na zaidi.

Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) vinapendekeza chanjo kwa watoto wote wenye umri wa miezi 6 na zaidi.

Chanjo ya COVID-19 ni salama, ni ya bure na inafaa kwa watoto. Chanjo hizo zilichunguzwa na kuonyeshwa kuwa salama kabla ya kupendekezwa kwa watoto na vijana.

Kama vile watu wazima, watoto na vijana wa rika zote wanaweza kuugua sana kutokana na COVID-19, kuwa na matatizo ya kiafya ya muda mfupi na mrefu, na kueneza COVID-19 kwa wengine.

Hakuna njia ya kusema mapema jinsi watoto au vijana wataathiriwa na COVID-19. Wale walio na hali ya kimsingi ya kiafya au walio na mfumo dhaifu wa kinga wana uwezekano mkubwa wa kuugua kutoka kwa COVID-19. Lakini hata watoto wenye afya nzuri wameugua sana. Ndiyo maana chanjo ni muhimu sana.

Hata watoto ambao tayari wameambukizwa COVID-19 wanapaswa kupata chanjo kwa sababu inatoa ulinzi zaidi. Inawezekana kupata COVID-19 zaidi ya mara moja, na kwa sababu tu mtu alikuwa na ugonjwa mdogo haimaanishi kuwa itakuwa hivyo tena.

Chanjo ya COVID-19 haisababishi ugonjwa wa COVID-19. Baadhi ya madhara, kama vile mkono kuuma au homa kidogo, ni ya kawaida baada ya chanjo na hupotea baada ya siku moja au mbili.

Chanjo ya COVID-19 husaidia kulinda familia na jamii dhidi ya COVID-19.

Mtoto wako atahitaji vipimo vyote vilivyopendekezwa vya chanjo ya COVID-19 kwa ulinzi bora zaidi - hii inaweza kujumuisha dozi za nyongeza.

Chanjo kwa watoto wadogo ni dozi ndogo kuliko chanjo kwa watoto wakubwa na watu wazima. Ukubwa wa kipimo cha chanjo inategemea umri wa mtoto, si ukubwa au uzito wao.

Ikiwa mtoto wako ana mhudumu wa afya, anaweza kukupa maelezo zaidi na kukusaidia kuratibu dozi zote zinazopendekezwa wakati wa kupata dozi ya kwanza. Watoto wanaweza kupata chanjo ya COVID-19 na chanjo zingine wanazohitaji wakati wa ziara hiyo.

Ikiwa mtoto wako hana mhudumu wa afya, unaweza kutembelea [mn.gov/vaxforkids](https://mn.gov/vaxforkids) kwa maelezo zaidi na kutafuta maeneo ya chanjo karibu nawe. Nambari ya simu ya dharura ya Idara ya Afya ya Minnesota kuhusu COVID-19 inapatikana pia ili kujibu maswali, na watu wanapatikana kuzungumza nawe katika lugha nyingi. Piga simu kwa 1-833-431-2053.

Tembelea tovuti ya Idara ya Afya ya Minnesota kwa [Rasilimali za Kupata Huduma ya Afya ya Gharama nafuu au Upate Bima ya Afya \(www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/materials/lowcost.html\)](https://www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/materials/lowcost.html) katika lugha nyingi.

[muziki wa kulisimua]

Minnesota Department of Health  
Communications Office  
PO Box 64975, St. Paul, MN 55164-0975  
[health.communications@state.mn.us](mailto:health.communications@state.mn.us)

10/19/2022 (Swahili)

Kupata habari hii kwa muundo tofauti, piga simu: 651-201-4989